**TAARIFA KWA UMMA**

# KWA WAAJIRI WOTE WALIOSAJILIWA NA MFUKO WA TAIFA WA BIMA YA AFYA

NATIONAL HEALTH INSURANCE FUND
NHIF
Dedicated to providing quality health care
ISO 9001:2015 CERTIFIED

## UWASILISHAJI WA ANKARA ZA MICHANGO YA KILA MWEZI

Itakumbukwa kuwa tarehe 7/9/2023, Mfuko ulitoa taarifa kupitia barua yenye Kumb. Na. DA.74/219/01-B/137 ya kuanza matumizi ya huduma mtandao (Online Employer Self Service Portal) iliyowawezesha waajiri wote, kuandaa ankara za malipo ya michango kwa ajili ya huduma za bima ya afya kwa wafanyakazi wao kila mwezi.

Hata hivyo, imebainika kuwa kuna baadhi ya waajiri wasioandaa Ankara kwa wakati. Hali hiyo husababisha usumbufu na malalamiko kwa wanachama na wategemezi wao wanakosa huduma kwenye vituo vya kutolea huduma za matibabu kutokana na michango kutolipwa kwa wakati.

Hivyo Mfuko unawakumbusha Waajiri wote waliosajiliwa kufanya yafuatayo:-

a. Kuandaa ankara ya michango ya kila mwezi kabla ya tarehe ya mwisho wa mwezi husika. Waajiri watakaoshindwa kuandaa ankara ya mwezi husika hadi kufikia tarehe 5 ya mwezi unaofuata watakosa huduma hadi hapo watakapoandaa ankara hizo;
b. Kulipa michango ya kila mwezi ndani ya kipindi cha siku 30 baada ya tarehe ya mwisho wa mwezi ya mchango husika. Hatua hii itawapa uhakika wa huduma wanachama pamoja na wategemezi wao na kuepuka tozo ya adhabu ya 5% ya michango husika ambayo haitalipwa;
c. Kutoa kwa wakati taarifa kupitia mfumo wa waajiri (online employer service portal) kuhusu wafanyakazi wapya walioajiriwa pamoja na waliokoma ajira;

Hatua hizi zinalenga kupunguza malalamiko ya wanachama na wategemezi wao kukosa huduma kutokana na baadhi ya waajiri kutozingatia taratibu za kulipa michango ya kila mwezi. Ofisi za Mfuko nchi nzima ziko tayari kutoa usaidizi endapo Mwajiri atahitaji msaada wakati wowote.

Imetolewa na;
**Idara ya Uhusiano na Mawasiliano kwa Umma**
23/05/2025